# Hashuki mtu hapa!

## Katiba, Ardhi na Maendeleo



Kitabu hiki kimetolewa na **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)** ikishirikiana na **Twaweza.**

**Waandishi:** Anna Henga, Evarist Kamwaga na Al-Amin Kheraj

**Wahariri:** Helen Kijo - Bisimba, Rakesh Rajani na Risha Chande

**Mchoraji:** Marco Tibasima

**Anuani:**

SLP 75254, Dar es Salaam.
Simu: 2773048/ 2773038
Nukushi: 2773037
Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz
Tovuti: www.humanrights.or.tz

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili na kutuma nakala mbili kwa LHRC.

# Utangulizi

Msomaji,

Wengi tumekua tukisoma au kusikia Katiba. Zaidi ya hayo, wengi tukadhani neno au dhana hii haituhusu bali ni maalumu kwa wanasheria au wasomi tu. Ukweli ni kwamba, Katiba ni kitu muhimu mno. Kama msingi ulivyo na umuhimu katika ujenzi wa nyumba, kadhalika na Katiba ni muhimu sana kwa Taifa na watu wake. Pia ina uhusiano wa moja kwa moja na maisha yetu ya kila siku.

Kijitabu hiki kitakuwezesha kutambua maana na umuhimu wa Katiba yaani jinsi inavyogusa maisha yako. Pia kinatoa mfano wa matukio kuhusu baadhi ya harakati za wananchi waliojitolea kuzilinda haki zao za kikatiba.

Ni mategemeo yetu kuwa msomaji licha tu ya kuburudika, utajifunza na kuishi kwa mujibu wa miongozo ya Kikatiba. Zaidi ya hayo, utawashirikisha na wengine elimu uliyopata katika kijitabu hiki.

**Dr. Helen Kijo Bisimba**
*Mkurugenzi Mtendaji - LHRC*

# Wahusika



**Mama Sikujua** - Mmiliki wa saluni



**Rehema -** Mfanyakazi saluni





**Paulo** - Mchuuzi wa vipodozi



**Mama Masanja (Betty)** - Mteja 1



**Mama Kashinde** - Mteja 2


Saluni asubuhi...
Naomba mnisuke ila leo sina hela, nitakulipa mwisho wa mwezi.
Kwanini?
Betty utanilaumu tu. Bila pesa, hapana!
Nadhulumiwa kila siku!



Mama nitafanyaje jamanii!
Nini tena mama? Msiba?
Mwanao yuko wapi?


Mgambo wametuvamia. Wanatutoa kwenye nyumba zetu kwa nguvu!
Kha! Wako wapi hao?


Hapo mtaani kwangu. Eti wanapitisha li-barabara lao kwenye makazi yetu.
Barabara! Ndo waharibu mali za watu?


Wanadai mji unakua, barabara za kisasa zinatakiwa.
Enhe, na kuhusu fidia?


Hakuna. Hata taarifa hatukupewa!
Si kuna sheria lakini? Twende tukawazuie!
Unaota! Unafikiri tuko Ulaya hapa? Lakini tukajaribu...


Eneo la tukio...


Nashema shuka upeshi! Au tukuporomoe?! Ushishezee mamlaka!


Paulo, inakuwaje wanatunyanyasa hivi?
Pole mama. Tumepata wafadhili kwa huu mradi. Ni bahati!


Lakini watu hawa hawana makosa, hawakupewa notisi
Ndiyo, wanaumia sasa hivi. Mbona watachekelea barabara ikikamilika!


Paulo unathubutu kutamka hivyo? Si kiduka chako nacho kimevunjwa!?
Sawa lakini biashara yangu itakua. Watu wengi watatumia barabara mpya ...pia wazungu watakuja kupaka rangi kucha zao hapa!


Paulo, maskini hawa hawakupewa taarifa. Kuna haki hapo?
Lazima tukimbizane na upepo wa maendeleo. Tuunge mkono juhudi za Serikali.


Na kama hatukubaliani na njia wanayotumia kuleta hayo maendeleo?
Serikali inawathamini. Msihofu. Imeweka mahakama kuwatatulia migogoro yenu.
Tena kweli! Tunaweza kupeleka madai yetu mahakamani.


Tukafungue kesi?
Tangu lini kuna haki mahakamani!
Itapatikana tu! Sina pa kulala. Kodi za nyumba sitazimudu. Naenda.


Kabisa! Pia kutofuatwa kwa taratibu za kisheria.
Dai letu la kwanza ni fidia za mali zetu...


Inatokea kila dakika. Mjomba wangu alifanyiwa hayahaya huko kwenye migodi yao.
Hivi hakujawahi kuwa na kesi kama hii huko nyuma?


Mmesahau yanayowapata baadhi ya wakulima? Wanaondolewa eti kupisha mashamba makubwa.
Nishawaambia barabara hii itaongeza mapato ya nchi. Kodi!


Sitajali uzuri wake kama wanavunja haki za binadamu. Hii ni kodi kubwa kuliko pesa!
Acheni ubinafsi! Barabara hii itasaidia wakulima kuuza mazao sokoni.


Huwezi halalisha matumizi ya mabavu kuleta mema. Tuna haki ya kuishi. Tutaidai pia.
Ndiyo!
Unafikiri kwanini wafadhili wametaka barabara hii? Na haraka hiyo imetoka wapi?
Hayo yanatuhusu nini wananchi? Tuwaachie viongozi wetu.


Paulo, tumia akili. Maslahi ya wananchi kwanza!
Nakubali. Rehema, tumeongea sana twendeni.


Siku chache baadae mahakamani...


Ni wazi taratibu hazikufuatwa. Mahakama inaamuru wadaiwa yafuatayo:
Walipe fidia kamili ya mali zilizoharibiwa na ya kuvunja haki za kiutu...
Wagharimie matibabu ya wote waliojeruhiwa...


Tatu, Halmashauri iwatafutie viwanja waathirika wote.
Mwisho, ujenzi wa barabara usitishwe mpaka hayo yametimizwa. Kesi imefungwa.
?!


Baada ya miezi sita...
Hehe! Naona sura zenu zimejaa tabasamu, karibuni.
VIPODOZI
Saana tu! Nimeanza kujenga nyumba. Barabara yetu ikamilike sasa!


Na mie nimefurahi. Natamani Katiba yetu iweke mpaka kati ya haki za msingi na maendeleo.
Ndiyo! Iseme 'bila wananchi husika kuridhia, mradi wowote usifanyike'.


Tunataka Katiba itayolinda haki ya kumiliki mali na ardhi.
Katiba itabaki kijitabu tu kama sisi hatutakuwa tayari kulinda haki zetu wenyewe.
Naunga mkono.

# Nini kifanyike:

1. Haki zako zikivunjwa, mweleze kiongozi wa Serikali ya mtaa, washirikishe wanafamilia, marafiki na majirani.
2. Usijichukulie sheria mkononi, tafuta msaada wa sheria.
3. Kuwa tayari kutoa maoni yako na kuchukua hatua wakati wowote.
4. Uwe na uchachu wa mabadiliko katika jamii yako.

